


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | May -2026

EAJK

# Maana Kisemiotiki Na Kipragmatiki Za Ujumbe Katika Mabango Ya Afya

**Authors**

**Alice Khayali Mukoko [(1)]; Fridah Miruka [(2)]; Deborah Amukowa [(3)]**

**Main author's email: amkhayali2015@gmail.com**

**(1.2) Masinde Muliro University of Science and Technology, Kenya; (3) Maseno University, Kenya.**

**Cite this article in APA**

Mukoko, A. K., Miruka, F., & Amukowa, D. (2026). Maana kisemiotiki na kipragmatiki za ujumbe katika mabango ya afya. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, 5(1), 54-64. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.1011

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**

Received: 2026.03.21

Accepted: 2026.04.26

Published: 2026.05.28

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Makala hii inalenga kuchanganua maana kisemiotiki na kipragmatiki ya jumbe kwenye mabango ya afya. Licha ya matumizi yake katika mawasiliano ya umma, bado kuna changamoto katika uelewa wa kina wa jinsi maana zinavyoundwa na kufasiriwa. Utafiti ulichunguza kwa kina miundo ya ishara inayotumika kwenye mabango ya afya na mchango wa muktadha katika uundaji wa maana. Mabango yalitokana na vituo vya afya vya kiwango cha pili vya serikali. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1986) na kuendelezwa na Clark (1996) pamoja na Nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na Saussure (1916) na kuendelezwa na Peirce (1931-1958). Nadharia ya Uhusiano ilitumika kueleza jinsi maana zilivyofasiriwa kwa kuzingatia muktadha, huku nadharia ya semiotiki ikitumika kuchanganua ishara. Muundo wa utafiti ulikuwa wa kiuchanganuzi kwa kutumia data za kithamano. Usampulishaji ulikuwa kimakusudi kwa mabango yaliyoandikwa kwa Kiswahili katika vituo hivyo. Data zilikusanywa kwa usomaji wa kina wa nyaraka na mabango, na kuchanganuliwa kwa mbinu ya uchambuzi wa yaliyomo. Matokeo yalionyesha kuwa rangi zilitumika kisemiotiki kuwasilisha taarifa mbalimbali, huku picha zikiimarisha ujumbe. Kipragmatiki, maana ya ujumbe ilitegemea muktadha. Msamiati ulipata maana mpya kulingana na muktadha wa matumizi. Rangi na picha vilitumika kimakusudi kuimarisha maana ya jumbe. Utafiti unahitimisha kwamba wabunifu wa mabango wanapaswa kutumia rangi na ishara wakizingatia maana yake kisemiotiki na kitamaduni. Matokeo yanatarajiwa kuwasaidia wabunifu wa mabango ya afya na wataalamu wa mawasiliano kuimarisha sera na mipango ya afya ya umma.

**Maneno muhimu:** Mabango ya afya, picha, pragmatiki, rangi, semiotiki.

## UTANGULIZI

Tafiti nyingi zimeangazia mabango kama chombo cha mawasiliano bila kuchunguza kwa kina maana za kisemiotiki na kipragmatiki za picha na ishara zinazotumika katika mabango ya afya. Kwa mfano, Oyebode na Onuabonah (2013), katika uchanganuzi wao wa kimaltimodali wa mabango ya afya, walibainisha namna ishara zilitumika kuwasilisha ujumbe. Aidha, Peija (2018) alibainisha mabango ya afya kuwa chombo muhimu cha mawasiliano, huku Nugraha na Haq (2021) wakithibitisha umuhimu wa mabango hayo katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Tafiti hizi hazikushughulikia kwa kina maana za kisemiotiki na kipragmatiki za picha na ishara, hali inayodhihirisha kuwepo kwa pengo la utafiti.

Mabango ya afya ni mojawapo ya mbinu muhimu zinazotumiwa katika mawasiliano ya afya. Yanategemea mchanganyiko wa picha, rangi, maandishi na alama ili kuwasilisha ujumbe. Hata hivyo, bado kuna changamoto katika uelewa wa kina wa namna maana za mabango hayo zinavyoundwa na kufasiriwa. Hivyo, lengo la makala hii ni kuchanganua maana kisemiotiki na kipragmatiki ya jumbe kwenye mabango ya afya.

Matumizi ya rangi kisemiotiki yamekuwa uwanja maalumu wa uchunguzi katika taaluma ya mawasiliano. Rangi haichukuliwi tu kama kipengele cha mapambo pekee, bali huchukuliwa pia kama ishara yenye maana inayochochea fasiri mbalimbali kutegemea muktadha wa kijamii na kitamaduni (Kress & van Leeuwen, 2021). Kwa mtazamo wa kisemiotiki, rangi hutumika katika ufasiri wa mabango. Koller (2008) anaeleza kwamba rangi hutekeleza wajibu wa kuelekeza macho ya msomaji kwenye sehemu muhimu za ujumbe. Machin na Mayr (2012) wanadai kuwa rangi hufanya kazi pamoja na maandishi na picha ili kuwasilisha taarifa fulani. Katika mabango ya afya, rangi zinazovutia macho hutumika kuvutia umakini wa hadhira na hivyo kuchangia katika kufanya ujumbe ukumbukwe.

Kulingana na nadharia ya Semiotiki (Peirce, 1931–1958), mawasiliano hufanyika kupitia ishara. Ishara hizi zimegawika katika ikoni, indeksi na alama. Ishara hizi hubeba maana inayofasiriwa kulingana na uhusiano wake na kile kinachowasilishwa. Rangi, picha, alama na maandishi yaliyotumika kwenye mabango ya afya huunda mfumo wa ishara unaoweza kuchunguzwa ili kutambua maana zinazowasilishwa. Hata hivyo, maana ya ujumbe kwenye mabango haiwezi kueleweka kikamilifu kwa kujikita kwenye uchambuzi wa ishara pekee, bali inategemea pia muktadha wa matumizi wa ishara hizo. Kulingana na Sperber na Wilson (1986), katika nadharia ya Uhusiano, maana hutokana na mchakato wa kiakili wa kutafuta fasiri iliyo na manufaa zaidi kwa juhudi ndogo, kwa kuzingatia muktadha wa ujumbe. Kwa hivyo, uchambuzi wa kipragmatiki katika utafiti huu unazingatia namna maana inavyoibuka kutokana na mwingiliano kati ya ishara na muktadha uliopo. Makala hii inathibitisha kuwa maana ya ishara katika mabango ya afya inategemea muktadha wa matumizi.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Kwa mtazamo wa kimataifa, tafiti zinaonyesha kuwa mabango ya afya hutegemea matumizi ya rangi, picha na maandishi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Rosil (2018) anaeleza kuwa matumizi ya rangi zinazovutia, picha zinazoeleweka kwa urahisi, na maandishi mafupi husaidia kuongeza ufanisi wa mawasiliano. Aidha, Odebunmi (2006), akinukuliwa na Ghevolor (2023), anasisitiza kuwa muktadha ni kipengele muhimu katika kuelewa maana ya ujumbe, kwani maana haiwezi kutenganishwa na mazingira ya matumizi. Hata hivyo, licha ya mchango huu, tafiti nyingi za kimataifa zimeishia kueleza umuhimu wa vipengele hivi bila kuchambua kwa kina jinsi maana hujengwa na kubadilika kulingana na muktadha. Hali hii inaonyesha umuhimu wa kuchunguza kwa kina uhusiano kati ya ishara na muktadha.

Katika muktadha wa Afrika, watafiti wameanza kuonyesha kuwa maana katika mabango ya afya hutokana na ushirikiano wa vipengele vya kisemiotiki. Ezirim na Aworo-Okoroh (2023) wanaeleza kuwa rangi, picha na lugha hufanya kazi pamoja katika kujenga maana, badala ya kila kipengele kufanya kazi kivyake. Vile vile, Madibaa na Lesitaokana (2025) katika utafiti wao nchini Botswana wanabainisha kuwa vipengele hivi huongeza uelewa wa ujumbe wa afya kwa jamii. Pamoja na mchango huo, tafiti hizi bado hazijashughulikia kwa undani jinsi muktadha unavyoathiri fasiri ya ishara hizo, na hivyo kuacha pengo katika uelewa wa mchakato wa ujenzi wa maana.

Aidha, utafiti wa Ingolo na Ong'onda (2024) kuhusu mabango ya UVIKO-19 nchini Kenya ulibainisha kuwa matumizi ya rangi, picha na maandishi yalichangia kuboresha uelewa wa ujumbe wa afya kwa wananchi. Hata hivyo, kama ilivyo katika tafiti za kimataifa na za Afrika kwa ujumla, utafiti huu ulijikita zaidi katika kueleza mchango wa vipengele vya kisemiotiki bila kuchunguza kwa undani namna maana huundwa na kufasiriwa katika mazingira halisi ya matumizi ya mabango hayo. Hali hii inaonyesha kuwa bado kuna ukosefu wa tafiti zinazochunguza kwa kina uhusiano kati ya ishara na muktadha wa matumizi.

Kwa mujibu wa mapitio haya, ni wazi kuwa tafiti nyingi zinaonyesha kuwa mabango ya afya ni mifumo ya kisemiotiki inayotegemea mwingiliano wa rangi, picha na maandishi katika kujenga maana. Hata hivyo, pengo kubwa linaonekana katika kutokuwepo kwa uchambuzi wa kina kuhusu jinsi maana hujengwa na kufasiriwa kulingana na muktadha wa matumizi. Kwa msingi huo, utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza kwa undani uhusiano kati ya ishara na muktadha katika ujenzi wa maana kwenye mabango ya afya.

**Nadharia za Utafiti**

Nadharia ya Semiotiki ya Peirce (1931–1958) na Nadharia ya Uhusiano ya Sperber na Wilson (1986) ndizo zilizoongoza utafiti huu. Nadharia ya Semiotiki ilitumika kuchanganua ishara kwa kuzingatia vipengele vitatu: alama, ikoni na indeksi. Alama ni ishara ambazo maana yake hutegemea makubaliano ya kijamii. Ikoni ni ishara zinazofanana moja kwa moja na kitu kinachowakilishwa. Indeksi ni ishara zinazohusiana moja kwa moja na kitu kinachorejelewa. Vipengele hivi vilimwezesha mtafiti kuelewa namna maana huundwa kupitia maandishi, picha, rangi na alama katika mabango ya afya. Kwa upande mwingine, Nadharia ya Uhusiano ilitumika kueleza namna ujumbe ulivyofasiriwa kutegemea muktadha na maarifa ya awali ya msomaji. Nadharia hii inasisitiza kanuni ya uhusiano ambapo mpokeaji hutafuta maana yenye faida kubwa kwa juhudi ndogo ya kiakili, pamoja na kanuni ya utambuzi inayodai kuwa akili ya binadamu huelekea kuchagua taarifa zilizo na umuhimu mkubwa zaidi. Kwa pamoja, nadharia hizi mbili zilitumika kuchambua sio tu muundo wa ishara na ujumbe, bali pia jinsi ujumbe unavyofasiriwa katika muktadha tofauti.

## MBINU ZA UTAFITI


Muundo wa utafiti huu ni wa kiuchanganuzi uliotekelezwa kwa kutumia mkabala wa utafiti maktabani. Kwa mujibu wa Bryman (2004), data za sekondari hutoa msingi mpana wa uchambuzi katika tafiti zisizohitaji ukusanyaji wa data za moja kwa moja kutoka kwa washiriki. Data ilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa vitabu, makala za kitaaluma, ripoti za taasisi za afya, na mabango ya afya yaliyopatikana katika vituo vya afya vya serikali vya kiwango cha pili. Mabango yaliteuliwa kimakusudi kwa kuzingatia uhusiano wao na mada ya utafiti pamoja na uwezo wao kuwakilisha matumizi ya ishara. Katika ukusanyaji wa data, mabango yalipigwa picha na kuchambuliwa kwa kuzingatia muktadha na ujumbe wake mkuu. Matokeo yaliwasilishwa kupitia maelezo katika aya mbalimbali yaliyoambatana na picha za mabango.

Uchambuzi ulilenga kubainisha matumizi ya ishara kama ikoni, indeksi na alama, pamoja na namna zinavyojenga maana. Kipragmatiki, maana ilichunguzwa jinsi ilivyojitokeza kulingana na muktadha wa matumizi wa ishara hizo. Utafiti huu unaweza kuathiriwa na upendeleo wa uteuzi kwa kujikita katika mabango ya vituo vya afya vya serikali pekee, pamoja na uwezekano wa upendeleo wa fasiri ya mtafiti. Hata hivyo, hali hii ilipunguzwa kupitia uteuzi makusudi wa mabango, usomaji wa kina wa mara kwa mara, na ulinganishaji wa matokeo na maandishi ya kitaaluma ili kuongeza uaminifu wa uchambuzi.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Maana Kisemiotiki na Kipragmatiki ya Ujumbe wa Mabango ya Afya

Utafiti ulibaini kuwa maana za jumbe kwenye mabango haya hazikueleweka kikamilifu kwa kujikita kwenye semiotiki pekee, ufasiri wa ishara pia ulitegemea muktadha wa matumizi. Data ifuatayo imebainisha namna mitazamo hii miwili inavyotegemeana katika kufasiri maana za jumbe.




**Kielelezo 1 (B1): "Lishe Bora ni Afya Bora"**

Bango B1 lina maandishi "Lishe bora ni afya bora" yaliyoandikwa kwa rangi ya kijani kibichi. Lina picha za matunda mbalimbali na watu wanaokula kwa furaha. Kulingana na Peirce (1931–1958), ishara hufasiriwa kupitia ikoni, indeksi na alama. Katika bango hili, maandishi "Lishe bora ni afya bora" ni ishara ya alama kwa sababu maana yake inatokana na makubaliano ya kijamii kuhusu lugha. Picha za matunda ni ikoni kwani zinafanana moja kwa moja na vyakula halisi. Picha ya watu wanaokula wakiwa na furaha ni ishara ya indeksi kwa sababu inaonyesha uhusiano wa moja kwa moja kati ya ulaji wa vyakula bora na afya njema. Bango hili limetumia alama, ikoni na indeksi kwa pamoja kuunda maana iliyowazi kwamba ulaji wa matunda na mboga unasababisha afya njema na maisha yenye furaha. Aidha, picha ya watu kwenye bango inatoa taswira ya familia. Kupitia picha hii, ushirikiano wa jamii katika kujenga ufahamu kuhusu umuhimu wa lishe bora unabainika. Hii inaashiria kuwa afya si jukumu la mtu mmoja pekee, bali ni la jamii nzima.

Rangi zimetumika kisemiotiki kuimarisha ujumbe. Kulingana na Bateman na Wildfeuer (2020), rangi ni rasilimali ya kisemiotiki inayoshirikiana na ishara zingine kama maandishi na picha ili kuunda ujumbe wenye maana. Rangi ya kijani iliyotumika kwenye maandishi, mboga na saladi inawakilisha afya, uhai, matumaini na asili (Eco, 1976). Katika bango hili, rangi hii imetumika kuashiria afya njema, uhai na matumaini. Rangi nyekundu inayoonekana kwenye tufaha na nyanya inawakilisha nguvu, ari na uhai (Kress & van Leeuwen, 2006). Rangi hii inavutia macho na hivyo kutoa msisitizo wa haraka kwa mpokeaji, na pia inatumika kama ishara ya uhai. Rangi ya njano na machungwa kwenye ndizi na chungwa zinaashiria mwangaza, nishati na nguvu (Elliot, 2015). Katika bango hili, rangi hizi zinahusishwa na ustawi wa mwili. Rangi ya zambarau kwenye zabibu ni ishara ya utajiri na ubora (Eco, 1976). Imethibitisha ubora wa lishe na kinga ya mwili, ikihusishwa kijamii na wingi wa virutubisho na thamani ya chakula. Matumizi ya rangi hizi yanaunda maana ya pamoja inayohamasisha ulaji wa vyakula bora na inachangia katika kujenga uelewa wa kijamii kwamba mchanganyiko wa vyakula vyenye rangi nyingi huwa na afya bora.

Picha zimetumika kisemiotiki kuwasilisha ujumbe kuhusu ulaji wa vyakula vinavyoboresha afya na si vyakula vyovyote. Muktadha wa bango hili ni kituo cha afya, jambo ambalo lenyewe ni ishara kwamba ujumbe unalenga masuala ya afya na kuwashawishi watu kula vyakula vyenye virutubisho bora ili kuboresha afya zao.

Kulingana na Sperber na Wilson (1986), maana ya ujumbe "Lishe bora ni afya bora" haipatikani katika maneno pekee bali inategemea muktadha wa matumizi. Msomaji hufasiri ujumbe kwa kuzingatia mazingira na maarifa yake ya awali ili kupata maana yenye manufaa kiutambuzi. Koech (2013) anathibitisha kuwa maana hufasiriwa kulingana na muktadha. Hivyo, bila muktadha maana ya ujumbe inaweza kubaki finyu, lakini kwa kuzingatia muktadha, ujumbe hupata fasiri pana na sahihi zaidi.

Lishe bora kwa kawaida inaweza kurejelea chakula chochote kizuri na safi. Hata hivyo, katika muktadha wa kituo cha afya, lishe bora ina maana pana zaidi kwani inarejelea vyakula vyenye aina zote za virutubisho muhimu katika kuimarisha afya ya

binadamu. Ni wazi kuwa muktadha una jukumu kubwa katika ufasiri wa ujumbe.




**Kielelezo 2 (B2): "Kinga ni Bora Kuliko Tiba"**

Katika bango B2 kuna maandishi "Kinga ni bora kuliko tiba" pamoja na picha zinazoonyesha mtu amelala ndani ya chandarua, mbu ndani ya chupa, mbu anayeonekana kuangamizwa, na mtu aliyevaa barakoa. Kulingana na Peirce (1931–1958), ishara hufasiriwa kupitia: ikoni, indeksi na alama. Picha ya mtu ndani ya chandarua na picha ya mtu aliyevaa barakoa ni ikoni kwani zinaakisi hali halisi. Picha ya mbu ndini ya chupa ni indeksi kwa sababu inaonyesha uhusiano wa moja kwa moja na chanzo cha ugonjwa (mbu husababisha malaria), huku chupa ikiashiria udhibiti. Maandishi "Kinga ni bora kuliko tiba" ni ishara ya alama kwani ni usemi unaokubalika kijamii na kitamaduni, unaomaanisha kuwa kuzuia ni njia bora ya kukabiliana na magonjwa kuliko kusubiri tiba.

Katika bango hili, matumizi ya rangi yanachukua nafasi muhimu ya ishara zinazoimarisha ujumbe wa afya. Rangi ya kahawia inayoonekana katika picha ya mbu ndani ya chupa na katika mandhari ya maandishi ni indeksi ya hatari na kifo cha mdudu, na pia ni alama ya onyo inayowakumbusha watazamaji umuhimu wa kuchukua tahadhari. Kwa mujibu wa Chandler (2017), rangi hubeba maana za kijamii na kihisia zinazovuka uhalisia wa kimaumbile. Rangi ya kahawia inaashiria dharura. Aidha, rangi ya bluu samawati inayoonekana katika picha ya mtu aliyelala ndani ya chandarua na mtu aliyevaa barakoa inawakilisha utulivu, usalama na afya (Kress & van Leeuwen, 2006). Rangi hii imetumika kujenga uhusiano chanya kati ya hatua za kinga na hisia za amani. Rangi nyeusi kwenye maandishi "Kinga ni bora kuliko tiba" inaimarisha ujumbe kwa kuupa msisitizo. Kwa mujibu wa Bateman (2014), rangi nyeusi ni ishara ya uzito na msisitizo wa maana. Kwa upande wa kipragmatiki, kulingana na Sperber na Wilson (1986), rangi hizi zinawapa watazamaji athari za moja kwa moja za kimuktadha bila kuhitaji juhudi kubwa ya kiakili. Rangi ya kahawia inachochea hisia ya hofu, bluu inaleta tumaini na usalama, huku nyeusi ikisisitiza uzito wa ujumbe. Hivyo, matumizi ya rangi katika bango hili ni muhimu sana.

Methali "Kinga ni bora kuliko tiba" imetumika kisemiotiki katika bango hili. Kwa kawaida inamaanisha ni busara kuchukua tahadhari mapema kuliko kushughulikia tatizo baadaye. Ili kufikia maana lengwa ya methali hii, ni sharti muktadha uhusishwe (Sperber & Wilson, 1986). Naye Ajayi-Osuolale (2017), akinukuu Odebunmi (2006), anaunga mkono kuwa muktadha ndio uti wa mgongo wa maana ya neno. Muktadha wa bango hili ukiwa kituo cha afya unaifanya methali hii kurejelea masuala ya afya. Maana yake inakuwa kwamba ni bora kujikinga dhidi ya magonjwa kuliko kungoja hadi kuugua ndipo upate tiba. Methali hii inawahimiza watu kuchukua hatua za kujitegemea ili kuzuia magonjwa.

Matumizi ya methali kwenye bango hili yameimarishwa na picha zinazoelekeza fikra za msomaji kwenye muktadha wa afya ya jamii. Kulingana na Achieng' (2009), picha zina ufanisi mkubwa katika kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Aidha, kulingana na kanuni ya Uhusiano (Sperber & Wilson, 1986), picha huchaguliwa ili kutoa uelewa mkubwa kwa juhudi ndogo ya kiakili. Picha ya mbu ndani ya chupa inaonyesha hatua ya kinga dhidi ya malaria.

Picha ya mtu aliyevaa barakoa inaashiria ulinzi dhidi ya magonjwa ya hewa kama UVIKO-19 na mafua. Picha ya chandarua inaonyesha kinga dhidi ya malaria kupitia matumizi ya vyandarua vyenye dawa, ambavyo ni njia rahisi na ya gharama nafuu ikilinganishwa na gharama za matibabu. Picha hizi zimechangia kuufanya ujumbe uwe wazi na kumwezesha msomaji kuelewa umuhimu wa kinga kupitia mifano halisi.




**Kielelezo 3 (B3): "Valia Boots, Usidungwe na Mwiba"**

Bango B3 linaonyesha picha ya jozi ya buti pamoja na maandishi "Valia Boots, Usidungwe na Mwiba." Jozi hii ya buti imewekwa katika mazingira ya shambani. Hizi ndizo ishara kuu zinazopatikana kwenye bango hili. Kulingana na Peirce (1931–1958), ishara zinaweza kufasiriwa kupitia aina tatu: ikoni, indeksi na alama. Katika bango hili, picha ya buti ni ikoni kwa sababu inawakilisha moja kwa moja kitu halisi, buti ndefu zinazotumika kulinda miguu. Hivyo, inaweza kuchukuliwa kama ishara ya kinga kwa ujumla. Kauli "Usidungwe na mwiba" ni indeksi kwani inaonyesha uhusiano wa moja kwa moja wa kisababishi kati ya kuvaa buti na kujikinga dhidi ya majeraha. Neno "mwiba" ni alama ya hatari na maumivu, na pia linaweza kuchukuliwa kama indeksi ya hatari, kwa mfano, maambukizi ya magonjwa ya zinaa au VVU. Hapa, "mwiba" umetumika kama fumbo la kitu chenye madhara kinachoashiria tishio kwa afya, huku buti ikiwa indeksi ya ulinzi dhidi ya hatari hiyo. Mazingira ya shamba yenye nyasi chache yanaimarisha ujumbe huu kwani yanawakilisha maeneo ambapo hatari ya kudungwa na miiba au vitu vyenye ncha kali ipo. Maneno "Valia Boots" ni alama ya kibiashara. Ni ishara ya kisheria inayotambulisha bidhaa fulani, na haina uhusiano wa moja kwa moja na buti yenyewe bali imejengwa kijamii na kiutamaduni kupitia muktadha wa biashara na matangazo. Katika muktadha huu, "Boots" imetumika kisemiotiki kumaanisha kondomu, ambayo ni kinga inayotumika kuzuia maambukizi.

Rangi zimetumika kwenye bango hili ili kuimarisha ujumbe. Kulingana na Kress na van Leeuwen (2006), rangi si kipengele cha mapambo tu, bali hubeba maana zinazotegemea muktadha wa matumizi (Chandler, 2017). Buti kwenye bango hili ni nyeusi. Rangi nyeusi, kwa mujibu wa Safavi (2023), imepanua maana zake kutoka kuashiria huzuni hadi kuwa ishara ya ubora, mamlaka na nguvu ya kijamii. Kipragmatiki, maana yake hubadilika kulingana na muktadha. Katika muktadha huu, rangi hii inahusishwa na uimara, uthabiti na kinga. Imetumika pia kusisitiza kuwa buti ni thabiti na inafaa kwa kazi ngumu mashambani. Kuna mstari wenye rangi nyekundu juu ya jozi ya buti. Kulingana na Barthes (1977), rangi nyekundu mara nyingi huashiria tahadhari, mapenzi au kejeli kutegemea muktadha. Katika muktadha huu, rangi hii ni ishara ya tahadhari na hatari. Inazua hisia kwamba kuna hatari (mwiba) na buti ndiyo kinga ya lazima. Rangi ya kijani hafifu cha nyasi na udongo inaakisi hali halisi ya maisha ya shambani na inaonyesha muktadha ambamo buti hutumika. Rangi ya kijani, kulingana na Eco (1976), ni ishara ya matumaini katika miktadha mingi ya kitamaduni. Katika bango hili, imetumika kuashiria matumaini iwapo "boot" itavaliwa. Kwa ujumla, rangi kwenye bango hili zimetumika kujenga

ujumbe wa tahadhari na kinga kwa kuhusiana moja kwa moja na mazingira ya shamba.

Picha katika bango hili imetumika kiisitiari. Sitiari ni mojawapo ya mbinu muhimu za kisemiotiki. Ili kuelewa maana yake, ni lazima muktadha uhusishwe. Kwa kuwa bango hili lilipatikana katika kituo cha afya, ujumbe wake unahusu masuala ya afya licha ya kutumia muktadha wa shambani. Ili kupata fasiri sahihi, msomaji anahitaji kuhusisha ujumbe na muktadha wa afya na maarifa yake ya awali (Sperber & Wilson, 1986). Msomaji anahitaji kuelewa maana ya neno "mwiba" na "boots" kisha kuyahusisha na muktadha wa afya. Koech (2013) anasema kuwa maana hufasiriwa kulingana na muktadha. Kwa kurejelea muktadha wa afya, ni wazi kuwa "mwiba" umetumika kiisitiari kuashiria hatari fulani ya afya, na ili kuepukwa ni sharti kutumia kinga ("kuvaa boots"), ambapo "boots" pia ni isitiari inayorejelea mpira wa kinga (kondomu). Hivyo, ujumbe kwenye bango hili, kwa kutegemea muktadha, una maana ya "Tumia kondomu ili ujilinde usije ukaambukizwa."




**Kielelezo 4 (B4): "Wanaume Wenye Busara Huvaa Soksi!"**

Bango B4 lina picha ya wachezaji wawili wanaocheza mpira uwanjani wakiwa wamevaa sare za michezo, soksi na viatu. Kuna pia maandishi "Wanaume wenye busara huvaa soksi" na nembo ya USAID. Kulingana na Peirce (1931–1958), ishara zinaweza kugawanywa katika makundi matatu makuu: ikoni, indeksi na alama, ambapo kila moja huchangia katika ufasiri wa ujumbe. Katika bango hili, picha ya wachezaji wa mpira ni ikoni kwani inaakisi moja kwa moja uhalisia wa mchezo wa mpira wa miguu. Mazingira ya mchezo yanabainika kupitia umbo, mavazi na ishara za wahusika. Soksi ambazo wachezaji wamevaa ni indeksi ya uchezaji wa mpira kwani zinahusishwa na soksi maalum za uwanjani. Hata hivyo, katika muktadha wa kiafya, soksi hizo zinachukua nafasi ya indeksi ya kinga. Hii inalingana na mtazamo wa Barthes (1977) kwamba ishara za kila siku zinaweza kubeba maana mpya kulingana na muktadha. Neno "soksi" katika maandishi "Wanaume wenye busara huvaa soksi" ni alama kwa sababu maana yake inatokana na makubaliano ya kijamii kutokana na kampeni za kiafya, ambapo linarejelea kondomu. Fasiri hii inaakisi kile Barthes (1991) alichokiita mambo ya kimaana, ambapo alama ya kawaida (soksi) inabadilishwa kuwa ishara ya msamiati wa kinga ya afya ya uzazi. Nembo ya USAID ni alama kwani ni chombo cha kimataifa. Aidha, inaashiria sehemu ya mradi mkubwa wa afya ya jamii unaoungwa mkono na shirika la kimataifa.

Rangi haijatumika tu kwa ajili ya mapambo, bali imebeba ujumbe maalum. Katika bango hili, mmoja wa wachezaji amevaa jezi jekundu. Kwa mujibu wa Kress na van Leeuwen (2006), rangi nyekundu huashiria hatari na onyo. Katika bango hili, rangi hii ni ishara ya hatari ya ngono bila kinga. Mchezaji mwingine amevalia jezi nyeupe. Kulingana na Altohami (2022), rangi nyeupe ni ishara ya mwanga, wema, usafi, kinga na afya. Maana hizi hutegemea muktadha wa matumizi. Katika muktadha wa bango hili, rangi nyeupe imetumika kama ishara ya kinga na afya inayohusiana na ujumbe wa kutumia kondomu. Uwanja wanaochezea una rangi ya hudhurungi

ambayo, kulingana na Manav (2007), huhusishwa na uchafu. Hivyo, rangi ya hudhurungi na nyeusi zinaashiria mazingira ya uwanja mchafu na kuchukua nafasi ya indeksi ya mazingira hatarishi ya maisha, na hivyo kukisisitiza haja ya kinga.

Picha imetumika kiisitiari kurejelea tendo la ngono. Hii ni mbinu ya kimafumbo na ya kimaadili. Hali hii inalingana na maelezo ya Wanyenya (2020) kwamba semi hutumika kufikisha mafunzo ya kijamii na kuhamasisha maadili bila kutumia lugha ya moja kwa moja ambayo huenda ikakiuka miiko ya kijamii. Sitiari ni mojawapo ya mbinu za kisemiotiki. Matumizi haya ya picha yamesababisha ujumbe usiwe wa moja kwa moja kwa sababu lugha ya moja kwa moja kuhusu matumizi ya kondomu mara nyingi huchukuliwa kama utovu wa heshima. Mchezo wa mpira umetumika kwa sababu unajulikana na kukubalika katika jamii. Matumizi ya muktadha wa mchezo huu yamechangia kuimarisha ujumbe na kuufanya uwe wa heshima na kukubalika katika jamii.

Ujumbe kwenye bango ni wa kisemiotiki. Mbinu ya isitiari imetumika ambapo neno "soksi" limetumika kurejelea kondomu. Mbinu hii ilitumika kuvutia umakini wa wasomaji na kuhimiza tabia chanya katika jamii. Maana fiche ya ujumbe huu inategemea muktadha na maarifa ya awali ya msomaji (Sperber & Wilson, 1986). Aidha, Mwenje na Kevogo (2023) wanaeleza kuwa maana za maneno hubadilika kulingana na muktadha. Hii inaonyesha kuwa maana ya neno "soksi" inabadilika kimuktadha. Bango hili lilipatikana katika kituo cha afya, jambo ambalo linathibitisha kuwa ujumbe unahusu masuala ya afya licha ya kutumia muktadha wa michezo. Uwepo wa nembo ya USAID unathibitisha kuwa ujumbe unahusiana na afya, kwani shirika hili linafadhili na kushirikiana na wizara ya afya katika kukabiliana na magonjwa ya ukimwi, kifua kikuu na malaria. Hivyo, msomaji anahitaji maarifa ya awali kuhusu majukumu ya USAID ili kufasiri ujumbe kwa ufanisi. Katika muktadha huu, "soksi" inarejelea kondomu, na picha ya wachezaji imechangia kuwasilisha ujumbe muhimu na mzito kuhusu kinga kwa njia nyepesi na chanya.

Kwa ujumla, ujumbe katika bango umepata maana mpya tofauti na maana yake msingi. Maana hii mpya imetokana na matumizi yake kimuktadha. Kulingana na Firth (1935), maana kamilifu ya ujumbe huwa ya kimuktadha na hakuna maana inayoweza kueleweka vizuri bila muktadha. Aidha, Anjejo (2015) akinukuu Lyons (1968) anasema kuwa maana na uamilifu wa neno au kauli hutokana na matumizi yake. Maana ya ujumbe kwenye bango imetokana na matumizi yake katika muktadha husika. Ni wazi kuwa muktadha ni muhimu katika ufasiri wa ujumbe, kwani maana ya kauli yoyote inatokana na matumizi yake badala ya maneno yenyewe pekee.




**Kielelezo 5 (B5): "Zimwi Limeingia Duniani. Epukana Nalo"**

Bango B5 lina maandishi ya Kiswahili na Kiingereza: "Zimwi limeingia duniani, epukana nalo / *A monster has entered the world, avoid it*." Bango hili lina taswira ya kivuli kikubwa cheusi cha 'zimwi' chenye utepe mwekundu kifuani na umbo dogo la binadamu linalosogea mbele kwenye barabara ya kijani. Ujumbe wake unahusu madhara ya VVU/UKIMWI na haja ya kuchukua hatua za kujikinga.

Kulingana na Peirce (1931–1958), ishara hutambuliwa kupitia: ikoni, indeksi na alama. Kivuli kikubwa cheusi ni ikoni ya zimwi, kwani kinafanana na kiumbe wa

kutisha katika fasihi ya Kiswahili na hivyo kuunda taswira ya hatari isiyozuilika. Umbo dogo la binadamu linalotembea mbele ni ikoni ya mhusika wa kawaida wa kijamii, likijenga athari ya ukubwa dhidi ya udogo. Athari hii inaonyesha udhaifu wa mwanadamu mbele ya tishio. Utepe mwekundu kifuani mwa zimwi ni indeksi ya ukimwi, kwa sababu unahusishwa kimataifa na kampeni za VVU na hivyo kuashiria moja kwa moja uwanja wa afya ya umma. Barabara ya kijani inayoelekea mbele ni indeksi ya mwelekeo au hatua, ikielekeza 'njia salama' ambayo huenda ikawa ni kupima na kutumia kinga. Maandishi "Zimwi limeingia duniani, epukana nalo" pamoja na tafsiri yake ya Kiingereza ni alama, kwani maana yake inategemea makubaliano ya kijamii na kitamaduni. Neno 'zimwi' linatokana na hazina ya fasihi simulizi ya Kiswahili na hutumika kitaswiria kutaja tishio lisiloonekana kwa urahisi, hivyo linahamisha maana hiyo kwa ukimwi kupitia mbinu ya uafikani. Matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza yamepanua hadhira na kuweka ishara katika mfumo mpana wa makubaliano ya kijamii (Kress & van Leeuwen, 2006).

Kress na van Leeuwen (2006) wanaeleza kuwa rangi ni mojawapo ya rasilimali za kisemiotiki. Katika bango hili, rangi nyekundu imetumika kwenye utepe. Rangi hii ni ishara ya hatari, nishati na onyo. Katika muktadha huu, inatumika kuashiria hatari, dharura na ukumbusho wa kimataifa kuhusu VVU. Rangi nyeusi imetumika kwenye kivuli kikubwa cha zimwi. Kulingana na Safavi (2023), rangi nyeusi imepanua maana zake kutoka kuashiria huzuni na kifo hadi maana mpya kama ubora na nguvu ya kujitegemea, kulingana na muktadha. Katika muktadha huu, rangi hii inawakilisha kifo na giza, ikibeba taswira ya adui asiyeonekana. Umbo dogo jeusi la binadamu linaashiria udhaifu wa mwili na hatari ya ugonjwa unaoweza kusababisha kifo iwapo hatua hazitachukuliwa. Rangi ya njano huashiria tahadhari, kama ishara za barabarani (Kress & van Leeuwen, 2006). Barabara ya kijani inaashiria matumaini na usalama, ikionyesha njia ya suluhisho kupitia kinga na upimaji. Kulingana na Machin (2007), rangi ya kijani huleta hisia za matumaini na uhai. Kwa ujumla, rangi hizi zimetumika kwa pamoja ili kujenga mkakati thabiti wa maana.

Picha na ujumbe kwenye bango zimetumika kiisitiari kurejelea jambo la kuogofya. Ili kupata fasiri lengwa, muktadha lazima uhusishwe. Khachula (2013) anahoji kuwa muktadha una mchango mkubwa katika kuchanganua maana ya ujumbe. Katui (2019) anaongeza kuwa maana ya ujumbe haiwezi kueleweka kwa kuzingatia maneno pekee bali inahitaji kuzingatia muktadha. Kulingana na Sperber na Wilson (1986), uelewa wa ujumbe hutegemea muktadha na maarifa ya awali ya msomaji. Taarifa mpya huchakatwa kwa kuilinganisha na maarifa ya awali. Muktadha wa bango ni kituo cha afya, hivyo ujumbe unahusu masuala ya afya. Katika muktadha wa kijamii wa Kiswahili, 'zimwi' ni kiumbe anayejulikana kuwa wa kutisha na anayehusishwa na hofu na maafa. Msomaji anahitaji maarifa ya awali kuhusu zimwi. Picha ya utepe mwekundu inathibitisha kuwa ugonjwa huu ni ukimwi, kwani ni nembo rasmi ya kimataifa inayotumika katika uhamasishaji wa VVU/UKIMWI (WHO, 2022). Hivyo, ujumbe huu umetumia taswira ya zimwi kiisitiari kuwakilisha ugonjwa wa ukimwi ulioenea duniani. Picha ya mtu anayeonekana akitoroka zimwi imetumika kiisitiari kuonyesha kuwa ugonjwa huo unastahili kuepukwa. Matumizi ya sitiari yamechangia kuufanya ugonjwa uonekane kama kiumbe halisi, na hivyo kuongeza athari ya kiutambuzi kwa msomaji kwa kuusisitiza hatari kubwa.

Muktadha wa bango uliongeza umuhimu wa ujumbe, kwani msomaji huuunganisha na ushauri wa kiafya anaouzoea. Kwa ujumla, bango limetimiza vigezo vya umuhimu kwa kuunganisha ishara rahisi, rangi kali na msamiati wa kitamaduni. Limetumia ishara, lugha na rangi ili kufanikisha lengo la kujenga ufahamu wa hatari ya kiafya kupitia taswira ya zimwi na rangi nyeusi, kutambulisha ugonjwa mahsusi kupitia utepe mwekundu, na kuelekeza hatua salama kupitia maandishi na barabara ya kijani.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho**: Uchunguzi huu unahitimisha kuwa mabango ni nyenzo muhimu katika utoaji wa elimu kuhusu afya kwa jamii. Rangi na picha zimetumika kimakusudi ili kuimarisha maana ya ujumbe. Aidha msamiati na jumbe zinapata maana mpya kutegemea muktadha wa matumizi. Aidha utafiti huu umechangia katika kuonyesha kuwa uchambuzi wa mabango ya afya unahitaji kuzingatia si tu ishara zilizotumika, bali pia muktadha unaoongoza fasiri ya maana zake.

**Mapendekezo:** Uchunguzi huu unapendekeza kuwa wabunifu wa mabango watumie rangi wakitilia maanani maana ya rangi hizo kisemiotiki.

**MAREJELEO**


Achieng', F. A. (2009). *Semiotic analysis of HIV/AIDS posters in Kenya* (Master's thesis, University of Nairobi). University of Nairobi Press.

Anjejo, M. O. (2015). *Uhamishaji wa maana katika sajili ya mchezo wa kandanda* [Master's thesis, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. https://ir-library.ku.ac.ke/items/46bf9d5d-f579-47ea-b9ad-be287d6dcc05

Altohami, W. M. A. (2022). A pragma-semantic analysis of colour terms in the Qur'an and their translations: The case of white and black. *Journal of Language and Linguistics Studies, 18*(1), 577–597. https://doi.org/10.52462/jlls.204

Aworo-Okoroh, J., & Ezirim, C. (2023). A pragmatic analysis of selected health posters in FCT Abuja. *Scholars International Journal of Linguistics and Literature, 6*(7), 1–? https://doi.org/10.36348/sijll.2023.v06i07.001

Barthes, R. (1964). Rhetoric of the image. In S. Heath (Trans.), *The responsibility of forms*. Blackwell.

Barthes, R. (1977). *Image, music, text*. Fontana Press.

Barthes, R. (1991). *Mythologies*. Hill and Wang.

Bateman, J. A. (2014). *Text and images: A critical introduction to the visual/verbal divide*. Routledge.

Bateman, J. A., & Wildfeuer, J. (2022). *Multimodality: Foundations, research and analysis*. De Gruyter.

Bryman, A. (2004). *Social research methods* (2nd ed.). Oxford University Press.

Chandler, D. (2017). *Semiotics: The basics* (3rd ed.). Routledge.

Clark, H. H. (1996). *Using language*. Cambridge University Press. https://doi.org/10.1017/CBO9780511620539

Eco, U. (1976). *A theory of semiotics*. Indiana University Press.

Elliot, A. J. (2015). Color and psychological functioning: A review of theoretical and empirical work. *Frontiers in Psychology, 6*, 368. https://doi.org/10.3389/fpsyg.2015.00368

Firth, J. R. (1935). The technique of semantics. *Transactions of the Philosophical Society*. Reprinted in J. R. Firth (1957), *Papers in linguistics*. Oxford University Press.

Ghevolor, A. J., Bassey, V. O., & Ekpang, J. N. (2023). Rhetorical strategies in selected Nigerian print media advertisements. *English Linguistics Research, 12*(2), 34–57. https://doi.org/10.5430/elr.v12n2p34

Ingolo, H. A., & Ong'onda, A. N. (2024). Health communication: A multimodal discourse analysis of selected coronavirus posters in Kenya. *African Journal of Empirical Research*. AJER Publishing.

Katui, J. (2019). *Mawasiliano ya wanafunzi wa vyuo vikuu kupitia Facebook* [Unpublished master's thesis]. Kenyatta University.

Koech, K. (2013). *Language use in social media among university students in Kenya* [Unpublished undergraduate research project]. Kenyatta University.

Koller, V. (2008). *Metaphor and gender in business media discourse*. Palgrave Macmillan.

Kress, G., & van Leeuwen, T. (2006). *Reading images: The grammar of visual design*. Routledge.

Kress, G., & van Leeuwen, T. (2021). *Reading images: The grammar of visual design* (New ed.). Routledge.

Lyons, J. (1968). *Introduction to theoretical linguistics*. Cambridge University Press.

Madibaa, G., & Lesitaokana, W. (2025). Semiotic analysis of visual elements in public health messages. *Health Literacy and Communication Open*. Taylor & Francis.

Machin, D., & Mayr, A. (2012). *How to do critical discourse analysis: A multimodal introduction*. Routledge.

Manav, B. (2007). Color-emotion associations and color preferences: A case study for residences. *Color Research & Application, 32*(2), 144–150. https://doi.org/10.1002/col.20294

Mwenje, L. S., & Kevogo, S. A. (2023). Athari za mabadiliko ya maana katika lugha ya Kiswahili: Mifano kutoka matini za kidini. *Kioo Cha Lugha, 21*(1), 75–91. https://doi.org/10.4314/kcl.v21i1.5

Odebunmi, A. (2006). *Meaning in English: An introduction to semantics and pragmatics*. Critical Sphere.

Peirce, C. S. (1931–1958). *Collected papers of Charles Sanders Peirce*. Harvard University Press.

Peirce, C. S. (1998). *Semiotics and significs*. Indiana University Press.

Rosil, H. (2018). The elements of poster design: Content visual analysis of Malaysian health campaign posters. *International Journal of Arts & Sciences Conference Proceedings*.

Safavi, S. (2023). Semiotic broadening of sign: A semiotic analysis of the black colour sign. *International Journal of Semiotics and Aesthetics*.

Sperber, D., & Wilson, D. (1986). *Relevance: Communication and cognition*. Harvard University Press.

Sperber, D., & Wilson, D. (1995). *Relevance: Communication and cognition*. Blackwell.

Wanyenya, W. (2020). *Matumizi ya lugha kwenye malezi ya watoto: Mfano wa matumizi ya semi katika jamii ya Wamasaaba nchini Uganda*. *East African Journal of Swahili Studies,* 2(1), 45–55. https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.151

World Health Organization. (2022). *World health report on the health situation*.